Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (http://www.al-islam.org)

15: Vita Juu Ya Kudhibiti Vyombo Vya Habari:

Jibu la kwanza la kisilika ambalo Myahudi atalitoa kutokana na kushutumiwa kabila lake kotoka kwa mtu asiye Myahudi ni lile la vurugu. Zilizotishiwa au zilizofanywa. Maelezo haya yatathibitishwa na mamia ya raia wa Marekani waliousikia ushahidi huo kwa masikio yao na kuona kwa macho yao.

Kama mchunguzi wa wazi wa Suala la Uyahudi atakuwa katika biashara, ‘kususia’ ni jibu la kwanza ambalo Wayahudi wanaelekea kulifikiria, iwe ni gazeti au biashara nyingine iliyoazishwa, au hoteli, au utengenezaji wa tamthilia au biadhaa yoyote ile iliyozalishwa ambayo mtengenezaji wake ametwaa sera ya ‘Bidhaa zangu ni za biashara lakini sio kanuni zangu.’ Kama kuna namna yoyote ile ya uhusiano wa kibiashara na wanafunzi wa Suala la Uyahudi, jibu la kwanza ni ‘kususia.’

Mbinu hii: ‘uendeshaji wa mnong’ono’ ilianza mwanzoni. Tetesi za kuhamanisha zilianza kuenea kwa nguvu na kwa haraka, “tusubirini tumshike” ndio maneno yaliyopitishwa. Wayahudi wasimamizi wa mashine zichapishazo habari za masoko ya hisa ya kitaifa wameanzisha wito wa “uvumi kwa siku.” Wakala wote wa vyombo vya habari wanaoongoza nchini Marekani wanadhibitiwa na Wayahudi.

Wakuu wa magazeti wa Kiyahudi wameanzisha sera ya ‘kichwa cha habari cha kukokoteza kwa siku’ Wayahudi wasimamizi wakuu wa vijana wauza magazeti mitaani ‘mitaa yote inayohusika imetwaliwa na ‘wafanyabiashara’ wa Kiyahudi ambao huwaruhusu tu vijana wao kuuza magazeti’, wanatoa amri ya kusisitiza habari fulani gazetini kwenye kelele zao za mitaani – ‘kelele mpya dhidi yake kila siku’. Kampeni nzima dhidi ya mkosoaji wa Uyahudi, yeyote yule atakayekuwa, huingia kwenye tishio, ‘tusubirini tumshike’.1

‘Msukumo wa mnong’ono’, ‘kususia’, haya ni majibu makubwa ya Wayahudi. Hali hii huunda ugumu na uchakavu wa hali ya akili katika watu wa mataifa ijulikanayo kama “Kuwahofia Wayahudi.”

Mapambano Ya Bw. Bennett

Hii ni hadithi juu ya mgomo iliyodumu kwa muda wa miaka kadhaa: Ni moja kati ya hadithi nyingi za aina hiyo hiyo ambazo zinaweza kuongelewa juu ya Marekani. Kumekuwepo na masuala mengine yaliyojitokeza zaidi baada ya hili, lakini hiyo inarudi nyuma kwenye mwanzo wa malengo na mamlaka ya Kiyahudi nchini Marekani, na ni moja ya mapambano

makubwa ambayo yalipiganwa na Wayahudi kwa mafanikio ili kuutokomeza uandishi wa habari wa kujitegemea.

Hadithi hii inahusiana na gezeti lililotoweka muda mrefu uliopita la ‘NewYork Herald’ gazeti ambalo lilikuwa libakie huru kutokana na ushawishi wa Kiyahudi jijini New York. Gazeti la Herald lilidumu kwa kipindi cha miaka 90, ambayo iliishia mnamo mwa 1920 kutokana na muunganisho ambao haukuepukika.
Lilikuwa ni gazeti lililofanya uhodari mkubwa kwenye ulimwengu wa ukusanyaji habari. Lilimpeleka Afrika Henry M. Stanley kumtafuta Livingstone. Liliunga mkono uchunguzi wa Jesnnette kwenye maeneo ya Arctic. Lilihusika kwa kiasi kikubwa na juhudi za usamabazaji wa nyaya za kupitishia habari kwenye bahari ya Atlantic.

Umaarufu wake miongoni mwa waandishi wa habari ulikuwa kwamba si taarifa zake wala habari zake kwenye maoni ya tahriri ambazo zingeweza kununuliwa au kushawishiwa. Lakini pengine uhodari wake mkubwa ulikuwa, kwa kipindi cha miaka mingi, ni kulinda uhuru wake wa uandishi habari dhidi ya mashambulizi ya pamoja ya Wayahudi wa New York. Mmiliki wake, Hayati James Gordon Bennett, raia mashuhuri wa Marekani aliyepata umaarufu kwa shughuli zake nyingi zenye msaada, kila wakati amekuwa na mahusiano ya kirafiki na Wayahudi wa Jiji hilo la New York. Kwa hakika hakuwa na chuki dhidi yao. Kwa kusema kweli hakuwahi kuwafanyia uadui kwa makusudi.

Lakini alikuwa amedhamiria kulinda heshima ya uhuru wa uandishi wa habari. Hakuwahi kuungana na sera ya kuwa watangazaji wanayo haki ya kutoa maoni yao juu ya sera ya uhariri wa gazeti ili kuleta ushawishi wa aidha kuyachapisha au kuyazima. Enzi za Bennett magazeti ya Marekani kwa wingi yalikuwa huru. Leo hii kwa ujumla wao yamo kwenye udhibiti wa Wayahudi. Udhibiti huu hutekelezwa kwa njia mbalimbali. Nyakati nyingine hutegemea hasa na jinsi mmiliki aonavyo umuhimu wake.

Lakini udhibiti upo, na kwa wakati huu ni uliokamilika. Miaka hamsini iliyopita mjini New York kulikuwepo na magazeti mengi sana kuliko yaliyopo hivi sasa, kwani muunganisho umepunguza ushindani kufikia machache tu ambayo hayashindani. Hali hii inalingana na ilivyo kwenye nchi nyinginezo, hasa Uingereza.

Gazeti la Herald la Bennett, linalouzwa kwa senti tatu, lilipendwa sana na lilikuwa ni chombo cha matangazo kilichopendwa sana kutokana na hali ya kusambazwa kwake. Kwa wakati huo idadi ya Wayahudi jijini New York ilikuwa ni chini ya theluthi moja ya ile iliyopo hivi leo, lakini kulikuwepo na mengi yaliyowakilishwa kwenye gazeti hilo.

Kwa wakati huu kila mtu wa magazeti analolifahamu ni kuwa: Viongozi wengi wa Kiyahudi wakati wote hupendelea amma kuchapisha hadithi gazetini au kuizima. Hakuna tabaka la watu wanaosoma magazeti ya umma kwa jicho makini sana kuhusiana na mambo yao wenyewe kama wasomavyo Wayahudi. Gazeti la Herald lilifuata tu sera hii toka mwanzo wa muundo huu wa unyanyasaji kwamba ilikuwa isiruhusuwe kuliyumbisha The Herald kutoka kwenye wajibu wake kama mhabarishaji wa umma. Na sera hii ilikuwa na fursa ya kujirejea kwa ajili ya magazeti mengine jijini humo.

Wakati ilipotokea kashfa kwenye vikundi vya kiyahudi (na mwishoni mwa karne ushawishi wa Kiyahudi uliokuwa unaendelea kukua nchini Marekani ulizizalisha kashfa nyingi) Wayahudi maarufu wangejazana kwenye ofisi za tahiriri za gazeti husika kwa lengo la kupanga mipango ya kuizuia hadithi hiyo.

Lakini wahariri walitambua kuwa gazeti la Herald haliwezi kuzuia chochote kile kwa ajili ya

mtu yeyote yule. Kuna manufaa gani kwa gazeti moja kuzuia na magazeti mengi mengine yasipozuia?

Hivyo basi wahariri wangesema: Tungefurahi sana kuizuia hadithi hii, lakni gazeti la Herald wataitumia, hivyo basi, nasi pia tutafanya hivyo hivyo ili kujilinda. Hata hivyo ikiwa mtalifanya Herald lizuie hadithi hiyo nasi pia tutafanya hivyo hivyo. Lakini Herald halikushindwa kamwe, amma kwa shinikizo la nguvu za ushawishi au kwa ahadi za kibiashara au vitisho vya kupoteza. Lilizichapisha hizo habari.

Alikuwepo mwenye benki mmoja wa Kiyahudi ambaye kila baada ya muda fulani alimtaka Bennett amuachishe kazi mhariri wa masuala ya kifedha wa gazeti la The Herald.

Bepari huyo mwenye benki alikuwa kwenye harakati za kutaka kuziondoa dhamana za Mexico kwa wakati ambapo dhamana hizo hazikuwa salama wa kutosha. Wakati ambapo kisasi kikubwa cha dhamana kilipokuwa kinataka kushushwa kutoka kwa wamarekani wasiogutuka, gazeti la Herald liliandika juu ya mapinduzi yanayotegemewa kutokea nchini Mexico na ambayo kwa hakika yalitokea. Yule mwenye benki huku akitokwa na povu mdomoni na kupendekeza kila ushawishi aliouweza ili kubadili watumishi wa uhariri wa masuala ya fedha ya gazeti la Herald, lakini hakufanikiwa kusababisha mabadiliko ya aina yoyote ile, hata ya mhudumu wa ofisi.

Wakati mmoja kashfa ya kutisha iliyomhusu mtu wa familia maarufu, Bennett alikataa kuizuia kwa madai kuwa kama tukio kama hilo lingetokea kwa familia nyingine yoyote ile maarufu mwa kabila lingine, lingechapishwa bila kuzingatia umaarufu wa watu waliohusika. Wayahudi wa Philadelphia walifanikiwa kupata uzuiaji huko, lakini kutokana na msimamo imara wa Bennett hakukuwa na uzuiaji jijini New York.

Gazeti ni jambo la kibiashara. Kuna baadhi ya masuala ambayo hayawezi kuguswa na gazeti bila kujiweka lenyewe kwenye hatari ya kuwa gazeti lililokufa. Huu ni ukweli kabisa kwa kuwa magazeti hayapati tena uungwaji mkono muhimu kutoka kwa jamii bali kutoka kwa watangazaji. Zile pesa ambazo msomaji analipia kwa kununua gazeti kwa shida sana hutosheleza kulipia karatasi nyeupe anayoipata. Kwa njia hii mtangazaji hawezi kudharauliwa tena kuliko viwanda vya karatasi vinavyoweza kudharaulika.

Kwa kuwa watangazaji wengi muhimu jijini New York walikuwa na bado wanaendelea kuwa na maduka makubwa, na kwa kuwa maduka makubwa mengi yalikuwa na bado yanaendelea kumilikiwa na Wayahudi, inatokea bila ubishi kwamba Wayahudi mara zote huwa wanao ushawishi kwenye sera za habari za magazeti wanayofanya nayo shughuli zao.

Kwa wakati huu, kila wakati imekuwa ni tamaa kuu ya Wayahudi kutaka kumchagua Meya wa Kiyahudi wa Jiji la New York. Walichagua wakati ambapo vyama vikuu vilivurugikiwa ili kuweka chaguo lao mbele. Mbinu walizotumia zilikuwa bainifu. Walifikiri kwamba magazeti yasingethubutu kukataa maamuzi ya mkusanyiko wa wamiliki wote wa maduka makubwa, kwa hali hiyo waliandika barua ya siri ambayo waliipeleka kwa wamiliki wote wa magazeti wa New York.

Wamiliki hao wa magazeti walikuwa wametatizika. Kwa siku kadhaa walijadiliana juu ya jinsi ya kufanya. Wote walikuwa kimya.Wahariri wa gazeti la Herald walimpelekea habari hizo kwa simu Bennett ambaye alikuwa ng’ambo kwa wakati huo, na alikuwa kwamba Bennett huyo huyo aliyeonyesha ushupavu na uwazi kwenye maamuzi ambayo yaliyomuanisha waziwazi. Alirejesha majibu ya simu hiyo: “Chapisheni hiyo barua.” Barua hiyo ilichapishwa kwenye The Herald. Kiburi cha watangazaji wa Kiyahudi kikawa

kimefichuliwa hadharani, ambapo wasio Wayahudi jijini New York walipumua kwa urahisi na kulisifia tendo hilo.2

Gazeti la Herald lilielezea kinaganaga kuwa haliwezi kuunga mkono mgombea wa maslahi ya kibinafsi, kwa kuwa lina msimamo wa kutetea maslahi ya jamii. Lakini viongozi wa Kiyahudi waliapa kulipiza kisasi dhidi ya The Herald na mtu ambaye alidiriki kuufichua mchezo wao.

Kwa hali yoyote ile hawakuwa wanampenda Bennett kwa muda urefu. Gazeti la Herald lilikuwa ndio “gazeti la jamii” hasa jijini New York, lakini Bennett alikuwa na kanuni kwamba ni yale majina ya familia za watu maarufu hasahasa tu ndio yachapishwe. Hadithi za majaribio ya Wayahudi matajiri wapya kujiingiza kwenye makala za kijamii za Herald, ni baadhi ya zile bora ambazo zinazotajwa na waandishi wa habari wa zamani.

Vita vyote vilianzishwa kwenye malumbano yaliyotokea kati ya Bennett na Nathan Straus, Mjerumani, Yahudi, ambaye nyumba ya shughuli zake za kibiashara ilijulikana kwan jina la R. H. Macy and Company, Macy akiwa ni Msikochi aliyeasisi biashara hiyo na kutoka kwa warithi wake ndiko Straus alikoipata biashara hiyo.
Straus alikuwa kama mtu mwenye ufadhili kwenye geto, lakini hadithi inaelezea kuwa kushindwa kwa Bennett kumtangaza kama mtu mwenye ufadhili ndiko kulikoanzisha uhasama, vita ndefu kwenye magazeti vilianza, mada yake ikiwa ni ulishaji kwa maziwa ni mazungumzo ya kipuuzi ambayo hakuna aliyeyatilia maanani isipokuwa Bennett na Straus.

Wayahudi, bila shaka walikuwa upande wa Straus. Wasemaji wa Kiyahudi walizunguka wakimwagia sifa nyingi kwenye mikutano na hadhara kadha na kumdhalilisha James Bennett. Bennett alisawiriwa kwenye shughuli mbaya na ovu sana ya kuwatesa Wayahudi wenye hadhi. Ilifikia hatua ambapo Wayahudi waliweza kuweka maazimio kwenye Baraza la Alderman.

Muda mrefu kabla, bila shaka, Straus mtangazaji mzito alikuwa ameondosha kila shughuli yenye thamani ya dola iliyokuwemo kwenye Herald. Kwa hivi sasa elementi zilizoungana na zenye nguvu za wayahudi wa mjini New York zilijikusanya ili kumpiga pigo la kumyumbisha Bennett. Sera ya Kiyahudi ya ‘miliki au haribu’ ilidhihirika na Wayahudi wakatangaza vita.

Wakiungana kama mtu mmoja, watangazaji wa kiyahudi wote waliyaondosha matangazo yao. Sababu yao kubwa ilikuwa ni kwamba gazeti la Herald lilikuwa likioneysha uadui dhidi ya Wayahudi. Madhumuni halisi ya hatua yao hiyo ilikuwa ni kumpondaponda mmiliki wa gazeti wa kimarekani aliyethubutu kutowategemea wao.

Pigo walilolitoa lilikuwa ni la kuyumbisha kweli. Lilimaanisha upotevu wa zaidi ya dola 600,000 kwa mwaka. Gazeti lingine lolote lile jijini New York lingelazimika kuacha biashara kutokana na upotevu huo. Wayahudi walilitambua hilo na walijiweka kando, wakisubiri kuanguka kwa mtu ambaye walichagua kumuona kama adui yao.

Lakini Bennett alikuwa mpiganaji. Isitoshe aliifahamu saikolojia ya Wayahudi vizuri zaidi, huenda kuliko mtu mwingine yeyote asiyekuwa Myahudi jijini New York. Aliyapindua mambo na kuyafanya magumu kwa wapinzani wake kwa mtindo wa kustaajabisha na usiotegemewa. Nafasi za maana za kuvutia kwenye magazeti yake mara zote zilikuwa zikitumiwa na Wayahudi.

Nafasi hizo mara moja alizibadili na kuwapatia wafanybiashara wasio Wayahudi kwa mikataba maalum. Wafanyabiashara ambao hapo awali walikuwa wamelundikwa kwenye

kurasa za nyuma na kona zilizofichika na Wayahudi matajiri zaidi, sasa waliinukia mbele ukurasa mzima katika sehemu maarufu zaidi. Mmoja wa wafanyabiashara asiye Myahudi ambaye alitumia fursa ya hali hiyo mpya alikuwa John Wanamaker, ambaye matangazo yake makubwa kuanzia wakati huo na kuendelea yalionekana kwenye magazeti ya Bennett.

Magazeti ya Bennett yaliondokea kuwa na usambazaji usio na kikomo na kurasa nzima za utangazaji. Mpango wa maangamizi uliopangwa vema kwa wakati huo haukutokea. Badala yake kulikuwa na mstukizo wa ucheshi kiasi. Hapa wakawepo wafanyabiashara wasio Wayahudi wa Marekani wakifaidi huduma bora zaidi za chombo cha utangazaji, huku wafanyabiashara wa Kiyahudi wakiwa bila uwakilishi.

Wakiwa wameshindwa kustahimili mchezo wa biashara kugeuziwa kwa wafanyabiashara wasio Wayahudi, Wayahudi walikwenda tena kwa Bennett wakiomba matumizi ya safu zake kwa ajiili ya kutangazia biashara zao.
Ule “Mgomo” uligeuka kuwa mgumu sana kwa wasusiaji. Bennett aliwapokea wote waliomwendea bila chuki. Walitaka warejeshewe nafasi zao za zamani, lakini Bennett akasema, Hapana! Walijadili sana, lakini Bennett akasema, Hapana! Walimpa mapesa mengi zaidi, lakini Bennett akasema, Hapana. Zile nafasi za ubora zaidi zilikuwa zimepotezwa.

Bennett alishinda, lakini ulidhihirika kuwa ni ushindi ghali sana. Wakati wote Bennett alikuwa anawakataa, wayahudi waliendelea kuwa na nguvu sana jijini New York, na walijawa na mawazo kwamba kudhibiti uandishi wa habari jijini New York kulimaanisha udhibiti wa mawazo wa nchini kote.

Idadi ya magazeti ilipungua kidogo kidogo kupitia kuunganishwa kwa matoleo. Adolph S. Ochs, Myahudi wa Philadelphia, alilichukua gazeti la ‘New York Times’. Mara moja alilifanya kuwa gazeti mashuhuri sana, lakini lililokuwa na upendeleo wa kuwahudumia Wayahudi. Ni sifa ya The Times kama gazeti hulifanya kuwa na uzito mkubwa mno kama chombo cha Kiyahudi. Kwenye gazeti hili Wayahudi husifiwa kila wakati, kutukuzwa na kulindwa; makabila mengine hayapewi hadhi ya aina hiyo.

Baada ya hapo Hearst akaingia ulingoni, mchochezi hatari sana huyu, kwa sababu sio tu kwamba anachochea mamabo yasiyo sahihi, bali pia kwa sababu huwachochea tabaka baya la watu. Alijizungushia mwenyewe genge la Wayahudi alioshawishika nao, akafanya kazi nao bega kwa bega, lakini hajazungumzia ukweli kuhusu wao; kamwe ‘hajawaangusha.’

Mwelekeo wa udhibiti wa Kiyahudi kwenye vyombo vya habari ulianza kwa nguvu, na umeendelea katika hali hiyo toka awali, majina ya zamani yakifanywa maarufu na wahariri mashuhuri na sera za Kimarekani, taratibu zikififia.

Gazeti huasisiwa amma juu ya akili kubwa mno ya kihariri, kwa hali ambayo huwa ni kielelezo cha mtu mwenye nguvu, au huwa linarasimishwa kama vile sera na kuwa la muundo wa kibiashara, kwa njia hii ya pili nafasi ya kuendelea kwake kudumu zaidi ya maisha ya wanzilishi wake ni kubwa.

Gazeti la Herald lilikuwa ni Bennett, na katika kupita kwake ilikuwa haiepukiki kwamba nguvu fulani na hadhi lazima viondoke kutoka kwenye gazeti hilo. Bennett akiwa mkubwa wa umri alihofia iwapo baada ya kifo chake gazeti lake lingeingia mikononi mwa Wayahudi. Alifahamu kuwa walikuwa wanaliangalia kwa hamu. Alifahamu kwamba wameziangusha au kuzitwaa na hatimae kuanzisha mashirika mengi ambayo yalithubutu kuongea ukweli juu

yao, na kusifia kuwa huo ulikuwa ni ushindi kwa Uyahudi.

Bennett alilipenda The Herald kama mtu ampedavyo mtoto. Hivyo alitayarisha wosia wake kwamba gazeti la Herald lisiangukie mikononi mwa mtu binafsi, lakini mapato yaingizwe kwenye mfuko utakowasaidia watu waliofanya kazi kulifanya Herald liwe kama lilivyokuwa.

Alifariki dunia mwezi Mei, 1919. Maadui wa kiyahudi wa Herald wakiwa wanaangalia kwa makini sana, kwa mara nyingine tena waliyaondoa matangazo yao, ili kulilazimisha, ikiwezekana kuliuza gazeti hilo. Walifahamu kwamba iwapo Herald litakuwa katika hali ya kushindwa, wadhamini wake hawatakuwa na njia nyingine ila kuliuza, bila kuzingatia wosia wa Bennett.

Lakini kulikuwepo pia baadhi ya watu jijini New York waliokuwa wameanza kuutambua ubaya wa magazeti ya Kiyahudi. Watu hawa walitoa kiasi cha fedha kwa ajili ya Herald kununuliwa na Frank A. Munsey.

Kisha, kwa mastaajabu ya wengi, Munsey alikoma kuliendeleza gazeti hilo maarufu, na kuliweka jina lake kama sehemu ya jina la ‘New York Sun’. Gazeti lililokuwa linaongozwa na Bennett limekufa. Watu waliokuwa wanafanya kazi wametawanyika huko ng’ambo kwenye nyanja ya magazeti, na kwa ujumla wao wamestaafu au kufariki.

Pamoja na hayo wayahudi hawakupata ulimiliki hasa wa The Herald. Angalau walifanikiwa tu kulioondosha uliongoni gazeti lingine lisilokuwa la Kiyahudi.
Walianza kapata udhibiti wa magazeti kadhaa; ushindi wao hivi sasa umekamilika. Lakini ushindi huo ulikuwa ni wa kifedha dhidi ya mtu aliyekwisha fariki. Ushindi wa kimaadili na hata wa kifedha pia ulibaki kuwa wa Bennett alipokuwa hai, ushindi wa kimaadili bado unabaki kuwa wa Herald. Ulidhihirisha ni nini kifanyike kwa akili zisizo na woga na zilizo huru, zikiungwa mkono na watu waliofahamu cha kutekeleza bila woga, akili huru zilizoungwa mkono na watu waliokuwa wanajua kazi yao na kuipenda kwa madhumuni yake.

Ilidhihirisha ni nini kinachoweza kufikiwa kama watu hawa wangeungwa mkono na wamarekani walio macho, mashughuli halisi, wasiokuwa wayahudi. Herald limepata uhai kwake kama kizuizi cha mwisho dhidi ya uyahudi jijini New York, na Marekani.

Hivi sasa Wayahudi ni watawala kamili zaidi wa nyanja ya uandishi wa habari jijini New York kuliko walivyo kwenye mji mkuu wowote ule huko Ulaya. Kwa hakika Ulaya mara nyingi hupokea magazeti ambayo hutoa habari halisi za Wayahudi. Hakuna hata moja huko mjini New York, na hivyo ndivyo hali itakavyobaki kuwa mpaka pale Wamarekani watakapojikurupusha kutoka katika usingizi wao wa muda mrefu, na kuangalia kwa macho makini ile hali ya kitaifa. Kuangalia huko kutatosheleza kuwaonyesha yote, na macho yao hayo hayo yatawatetemesha wavamizi hawa wa Mashariki.

Protokali ya Kwanza

“Ushindi wetu umefanywa kuwa rahisi kutokana na ukweli kwamba katika uhusiano wetu na watu tuliowahitaji, tumekuwa wakati wote tukifanya kazi kwenye hisia nyeti sana za akili ya binadamu, juu ya hesabu za fedha juu ya tamaa, juu ya kutotosheka na mahitaji ya mali kwa watu na kila moja ya udhaifu huu wa kibinadamu, ukichukuliwa peke yake inatosha kuidhoofisha hatua, kwa kuwa husalimisha utashi wa watu kwenye mpangilio wa yule ambaye amenunua shughuli zao.”

1. NENO LA MHARIRI: Kufuatia kupanda kwa ‘umashuhuri’ wa waandishi waliounganishwa kibiashara wa makala maalumu katika magazeti tangu 1920, sasa neno ni ‘pakaza matope’; hususani huonekana katika mambo ya habari - kisiasa.
2. Leo hii ni vigumu kumpata mwandishi thabiti na mwenye fikra huru kama huyu. Iwapo akatokea kama huyu, hatatokea haraka sana kama atakavyotoweka kwa njia ya muujiza wa ajabu, milele – Mhariri.

Source URL:
http://www.al-islam.org/sw/myahudi-wa-kimataifa/15-vita-juu-ya-kudhibiti-vyombo-vya-habari